


BETHSAIDA ORPHANAGE EDUCATION CENTRE

2024

# BETHSAIDA SECONDARY SCHOOL

Shule ya Kipekee ya Wasichana kwa watoto wanaotoka katika mazingira magumu na yatima - TANZANIA

# Report

VOL 1/2024

TANZANIA

# Yaliyomo

| | |
|---|---|
| Utangulizi | 03 |
| Dibaji | 04 |
| Vipaumbele vya Kituo | 05 |
| Thamira na maono ya kituo | 06 |
| Malengo ya Mradi | 07 |
| Mahitaji ya Kituo | 10 |
| Ufaulu wa Masomo | 11 |
| Makisio ya Bajeti | 15 |
| Hitimisho | 16 |

# Utangulizi

## BETHSAIDA ORPHANAGE EDUCATION CENTRE NI KITUO AMBACHO KIMEANDALIWA MAHUSUSI KWA LENGO LA KUSAIDIA WATOTO WA JINSIA YA KIKE WANAOISHI KWENYE MAZINGIRA MAGUMU.

Bethsaida Orphanage Education Centre (BOEC) ni kituo cha watoto yatima kilichoanzishwa rasmi mnamo mwaka 2005 kwa lengo la kutoa msaada kwa watoto yatima na wale wanaotoka katika mazingira magumu. Kituo hiki kinasimamia Shule ya Sekondari ya Bethsaida iliyopo Mpigi Magoe, wilayani Ubungo, Jiji la Dar es Salaam.

Shule hii ilianzishwa kwa madhumuni ya kuhakikisha watoto wenye mahitaji maalum, hasa yatima, wanapata fursa ya elimu bora. Hii ilitokana na changamoto kubwa ya watoto wengi wanaotoka kwenye mazingira magumu kukosa nafasi ya kupata elimu stahiki, hali iliyosababisha kuwepo kwa hitaji kubwa ya taasisi kama Bethsaida ili kusaidia katika kupambana na changamoto hizi na hatimaye kubadili maisha ya watoto hawa kupitia elimu.

Bethsaida Orphanage Education Centre(BOEC) imeendelea kukua na kuwa msaada muhimu kwa watoto hawa, ikiwapa matumaini mapya na fursa ya maisha bora kupitia elimu na malezi yenye upendo. Hadi sasa, kituo kimefanikiwa kuboresha maisha ya mamia ya watoto ambao pasipo kuwepo na shule hii wangekosa fursa ya kupata elimu na kujijenga kimaisha.

# Dibaji

## Kituo cha BOEC, kupitia shule yake ya Sekondari ya Bethsaida inapenda kuwasilisha mapendekezo ya miradi ya Shule

Kituo cha Bethsaida Orphanage Education Centre(BOEC) kupitia shule yake ya Sekondary ya Bethsaida ina kila sababu ya kujisifu kwa mafanikio makubwa ambayo yamepatikana tangu kuanzishwa kwake mwaka 2005. Taasisi hii imewezasha zaidi ya watoto 417 kuhitimu kidata cha nne. Aidha, zaidi ya asilimia 90% ya wanafunzi waliomaliza shule hii wameweza kuendelea na masomo katika vyuo mbalimbali hapa nchini. Tunatoa shukrani za dhati kwa Mhe.Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani. Dkt. Samia Suluhu Hassani kwa kuwa bega kwa bega nasi, Taasisi za kidini, wananchi, serikali, na wafadhili wa ndani na nje ya Nchi ambao wamechangia katika kufanikisha malengo haya.




Raymond Michael Machary (PMP)

**Mwenyekiti wa Kituo cha Bethdaisa Orphanage Education Centre**

Raymond Machary
Ph.D Candidate (DBA)
Chairman of Bethsaida Orphanage Education Centre
MSc Finance and Investment
MSc Project Planning and Management
MSc IT & Management
Certified PMP
Member of PMI
Certified Director by IoDT
Certified on National Procur e ment procedure
Trained by Catholic Jasuite Church
Expert in Python and Big data analytics and leadership

# Shukrani



Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hasan

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

“Mhe. Rais mnamo mwezi March 2021 siku ya mahadhimisho ya kilele  cha watoto Duniani aliwahamasisha  watanzania  kuwa na utamaduni wa kuwalinda, kuwajali na kuwapenda watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu”

# Vipaumbele vya Kituo

## Vipaumbele 10 vya shule ya Bethsaida

Bethsaida Orphanage Education Centre(BOEC) inayo vipaumbele mbalimbali vya kiutendaji, ambavyo ndio nguzo ya mafanikio ya kituo



### ELIMU BORA

Tunaweka mkazo katika kutoa elimu bora kwa watoto yatima na wale wanaotoka katika mazingira magumu, ikiwa ni pamoja na kuboresha vifaa vya shule na kuajiri walimu wenye ujuzi.


---



### HUDUMA ZA AFYA NA LISHE

Tumejikita katika Kuimarisha huduma za afya na lishe kwa watoto, ikiwa ni pamoja na kutoa chakula bora na huduma za matibabu.

---



### ULINZI NA USALAMA

Tunahakikisha  mazingira salama kwa watoto yanakuwepo, pia wanakuwa na ulinzi dhidi ya unyanyasaji na vitendo vya ukatili.

---



### MAFUNZO YA UFUNDI STADI

Tunawekeza katika Kutoa mafunzo kwa  ustadi kwa watoto ili kuwapa ujuzi wa vitendo watakaowasaidia katika maisha yao ya baadaye.

---

# Dhamira na Maono ya kituo

Dhamira

Kutoa msaada wa kijamii na kielimu kwa watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu, kwa lengo la kuwapa fursa ya kupata elimu bora, malezi, na uongozi unaowezesha kujenga maisha yao ya baadaye.

Maono

Kuwa kituo kinachoongoza katika kuboresha maisha ya watoto yatima na wale wanaokabiliwa na changamoto za maisha, kwa kuwapa mazingira salama na yenye upendo ambapo wanaweza kufikia malengo yao ya kielimu na kiutu kwa urahisi.





# Malengo ya Miradi

## Malengo ya Miradi ya BOEC kupitia Shule ya Sekondari ya Bethsaida.

Kituo cha Bethsaida Orphanage Education Centre (BOEC) kimejikita katika kusimamia na kuendeleza utoaji wa elimu bora katika Shule ya Sekondari ya Bethsaida. Malengo makuu ni pamoja na

### Malengo

| | |
|---|---|
| Kuhakikisha Upatikanaji wa Elimu Bora: : | Kutoa elimu bora kwa watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu, ili kuwapa fursa sawa za mafanikio katika jamii. |
| Kujenga Uwezo na Ujuzi: | Kuwawezesha watoto kupata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kujitegemea na kuchangia katika maendeleo ya taifa. |
| Kuimarisha Ushirikiano na Wadau: | Kukuza ushirikiano kati ya Bethsaida Orphanage Education Centre na wadau mbalimbali kwa lengo la kupanua wigo wa msaada na rasilimali. |
| Kuwezesha Afya na Ustawi: | Kuimarisha huduma za afya na ustawi kwa watoto, ili kuhakikisha wanakuwa na maisha bora na yenye afya njema. |

# Changamoto zinazowakabili Wasichana wanaotoka katika mazingira magumu

Wasichana yatima na wale wanaotoka katika mazingira magumu nchini Tanzania wanakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinazuia maendeleo yao ya kijamii, kielimu, na kiuchumi. Changamoto hizi ni pamoja na:

**Ukosefu wa Fursa za Elimu:** Wasichana wengi wanaotoka kwenye kaya maskini au yatima hukosa fursa ya kupata elimu bora kutokana na ukosefu wa ada, vifaa vya shule, na miundombinu ya kutosha. Hii inawafanya wengi wao kushindwa kumaliza masomo na hivyo kushindwa kupata ujuzi wa msingi unaohitajika kwa maisha yao ya baadaye.

**Ubaguzi wa Kijinsia:** Katika jamii nyingi, wasichana wanakumbana na ubaguzi wa kijinsia unaowanyima haki sawa na wavulana katika upatikanaji wa elimu na fursa za kiuchumi. Hii inaathiri kujiamini kwao na uwezo wao wa kufikia malengo yao.

**Afya Duni na Lishe:** Wasichana yatima na hata wale wanaotoka kwenye kaya masikini mara nyingi hukabiliwa na changamoto za kiafya na ukosefu wa lishe bora. Hali hii inaweza kuathiri maendeleo yao ya kimwili na kiakili, na kuongeza hatari ya magonjwa na udumavu.

**Ukosefu wa Ulinzi na Usalama:** Wasichana wanaoishi katika mazingira magumu wako katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa kijinsia, ndoa za utotoni, na unyonyaji. Ukosefu wa ulinzi unawaweka katika hatari ya kupata majeraha ya kimwili na kisaikolojia ambayo yanaweza kuwa na athari za muda mrefu.

**Ukosefu wa Msaada wa Kijamii na Kisaikolojia:** Wasichana yatima mara nyingi hukosa msaada wa kijamii na kisaikolojia kutokana na upweke, unyanyapaa, na hali ngumu za maisha. Hii inaweza kuathiri afya zao ya kiakili na uwezo wa kukabiliana na changamoto za maisha.

**Ukosefu wa Rasilimali:** Ukosefu wa rasilimali muhimu kama vile maji safi, vifaa vya kujifunzia, na huduma za afya hufanya maisha ya wasichana hawa kuwa magumu zaidi na kuwazuia kufikia uwezo wao kamili.





# Hali ya Miundombinu na Mahitaji ya Kituo

Kituo cha Bethsaida Orphanage Education Centre kimekuwa kikiendesha shughuli zake kwa kutumia miundombinu iliyopo, lakini kuna changamoto kadhaa zinazohitaji kutatuliwa ili kuboresha mazingira ya kujifunza na kuishi kwa watoto wanaoishi kituoni hapo.

## Hali ya Miundombinu

Hali ya miundombinu katika kituo inajumuisha majengo ya madarasa, mabweni, ofisi, vyoo, na maeneo ya burudani. Majengo haya, ingawa yanatumika, yanaonyesha dalili za uchakavu kutokana na muda mrefu wa matumizi bila ukarabati mkubwa. Vyoo vinahitaji pia ukarabati ili kuhakikisha usafi na afya ya watoto.

Aidha, kituo kinahitaji kuimarisha miundombinu ya maji safi na salama, miundombinu ya umeme, na mifumo ya maji taka ili kuhakikisha mazingira safi na salama kwa watoto. Kwa sasa, upatikanaji wa maji safi ni changamoto kubwa ambayo inachangia gharama kubwa za uendeshaji wa shule.



# Mahitaji ya Kituo

Kituo kina mahitaji muhimu ambayo yanapaswa kushughulikiwa ili kuboresha hali ya miundombinu na kuhakikisha kwamba watoto wanapata elimu na huduma bora. Baadhi ya mahitaji hayo ni pamoja na:

**Ukarabati wa Majengo:** Kituo kinahitaji ukarabati wa madarasa, mabweni, na majengo mengine ili kuhakikisha yanaendelea kutumika kwa ufanisi na kutoa mazingira mazuri ya kujifunza.

**Vifaa vya Shule:** Kuna upungufu wa vifaa vya kufundishia kama vile vitabu, vifaa vya maabara, na vifaa vya michezo. Hii inazuia watoto kupata elimu bora na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kujifunza.

**Maji Safi na Salama:** Uwekezaji unahitajika katika mabomba ya maji, matanki, na mifumo ya kusafisha maji ili kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa matumizi ya kila siku.

**Umeme na Mifumo ya Teknolojia:** Kituo kinahitaji kuboresha upatikanaji wa umeme wa uhakika pamoja na kuanzisha mifumo ya kiteknolojia kama vile kompyuta na mtandao wa intaneti ili kurahisisha wanafunzi kuweza kupata elimu ya kidigitali.

**Vifaa vya Afya na Usafi:** Kuna haja ya kuongeza vifaa vya afya na usafi, ikiwa ni pamoja na sabuni, vifaa vya kutibu maji, na huduma za matibabu kwa dharura wa ajili ya wanafunzi.

**Uhakika wa Mishahara ya Walimu na wafanyakazi:** Kituo kinatumia takribani TZS 18 Mil kwa ajili ya chakula na gharama za mishahara ya walimu na wafanyakazi wengine. Tunashauri uandaliwe utaratibu mzuri ambao utawezesha shule kuwa na uhakika kupata kiwango hiki cha fedha na hatimaye kuweza kujiendesha.


**Uhabaa wa madarasa kwa ajili ya kutoa elimu ya masomo kwa vitendo:** Kituo kimemejipanga vema katika kuhakikisha kuwa wanafunzi mbali na kupata elimu ya nadharia kwa maana ya CSEE basi pia wanapata elimu ya masomo ya vitendo “Vocation Training”

## Matokeo ya Ufaulu wa Shule Sekondari ya Bethsaida

Shule ya Sekondari ya Bethsaida inayosimamiwa na kituoa cha BOEC pamoja na kuwa ni shule mahususi ya watoto wa jinsia  ya kike wanaotoka katika mazingira magumu lakini imekuwa ni moja ya shule inayofanya vema katika matokeo ya kidoto cha nne kila mwaka. Hii ni ishara kuwa mafanikio haya yanasababishwa na usimamizi mzuri, weledi wa walimu na ushirikiano mzuri na jamii.

# Hali ya matokeo ya kidato cha Nne

Idadi ya watoto waliofanikiwa kupata fursa ya kuweza kuendelea na masomo baada ya kufaulu vizuri matokeo ya kidato cha nne




97% Asilimia ya ufaulu

3% Idadi ya watoto wanaopata division IV

Aidha, pamoja watoto wengi ambao huwa wanachaguliwa kujunga na shule ya Sekondari ya Bethsaida wanakuwa  hawajaandaliwa vema kimasomo, walimu wetu huwa wanafanya kazi ya ziada kuakikisha watoto wanaandaliwa vema ili waweze kuendana na kasi lakini wawe na weledi unaohitajika. Mambo ya awali ambayo huwa yanafanyika ni pamoja na


- Mafunzo ya Maadili  - Wanafunzi huwa wanaanza kufundisha masuala ya maadili.
- Wanafunzi wanafundishwa umuhimu wa kusali- Kila mtoto atalazimika kusali kulingana na imani yake.
- Kujifunza kuhusu usafi wa mazingira - Wanafunzi hupata mafunzo kuhusu usafi wa mazingira.




**Hali ya ufaulu wa watoto wanaosoma Shule ya Sekondary ya Bethsaida  - Tanzania**

# Matokeo ya Shule ya Sekondari ya Bethsaida.

Matoke ya shule ya bethsiada tangia kuanzishwa kwake mwaka 2005






# Maelezo ya Mradi wa Kituo(BOEC) kupitia shule ya Sekondari ya Bethsaida.

Mradi wa Bethsaida Orphanage Education Centre(BOEC) umeanzishwa kwa lengo la kusaidia jamii kwa kutoa elimu bora kwa watoto yatima na wale wanaotoka katika mazingira magumu. Tangu kuanzishwa kwake, zaidi ya watoto 417 wamefanikiwa kumaliza masomo yao katika Shule ya Sekondari ya Bethsaida. Hii ni ishara tosha kwamba mradi huu umekuwa na matokeo chanya kwa jamii, na umesaidia kubadilisha maisha ya watoto wengi wa Kitanzania.

Mafanikio haya yanaonyesha umuhimu wa mradi huu katika kuleta mabadiliko katika maisha ya watoto wengi ambao wangeweza kukosa fursa ya kupata elimu endapo kituo hiki kisinge kuwepo. Kwa sababu hiyo, ni muhimu kuhakikisha kuwa mradi huu unaendelea kuwepo na kuimarishwa ili watoto wengine wengi zaidi waweze kunufaika na fursa hii ya kipekee.

Mradi huu unalenga kutoa mazingira bora ya kujifunza na kuishi kwa watoto, kwa kuwapa elimu, ushauri, na huduma zinazohitajika ili waweze kujitengenezea maisha bora ya baadaye. Kituo cha Bethsaida kina dhamira ya kuendelea kuwahudumia watoto hawa kwa muda mrefu, na kwa kufanya hivyo, tunajenga msingi imara kwa maendeleo ya jamii nzima ya Watanzania.

## Malengo Mahususi ya Mradi

Malengo mahususi ya mradi huu ni kuwezesha watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu kupata fursa ya kusoma vizuri na hatimaye waweze kuwa sehemu ya kuchangia uchumi wa nchi yetu ya Tanzania. Kupitia elimu bora, watoto hawa wataweza kujenga msingi mzuri wa maisha yao ya baadaye na kuwa raia wenye manufaa kwa taifa.

Hata hivyo, changamoto kubwa tunazokabiliana nazo ni uhaba wa fedha za kuwasaidia watoto hawa katika kupata elimu. Mahitaji ya watoto wanaotakiwa kupata elimu katika Shule yetu ya Bethsaida ni mengi sana, na uwezo wa shule kwa sasa ni kupokea watoto zaidi ya 50 kwa kila mwaka. Hii ni idadi ndogo ikilinganishwa na mahitaji halisi ya jamii yetu.

Licha ya changamoto hizi, shule ina uwezo wa kupanua huduma zake kwa kujenga madarasa na vyumba vya kulala zaidi, hivyo kuongeza idadi ya watoto wanaoweza kupokewa hadi kufikia zaidi ya 400 kwa mwaka. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huu unakwamishwa na uhaba wa fedha, kwani shule hii inaendeshwa kwa asilimia zaidi ya 90% kutokana na michango ya wananchi na wadau mbalimbali.

Kwa sababu hiyo, tunahitaji msaada wa kifedha na rasilimali ili kufanikisha malengo haya na kuhakikisha kuwa watoto wengi zaidi wanapata fursa ya kupata elimu bora na kuboresha maisha yao.

# Makisio ya Bajeti

Huu ni mchanganuo wa bajeti ya vitu vinavyohitajika na kituo kupitia shule ya Sekondary ya Bethsaida. Aidha, Mahitaji haya ni ya awali ambayo tunaimani yatakuwa chachu katika kuboresha ufanisi katika utoaji wa elimu bora kwa watoto wengi zaidi wa kitanzania.

| Namba | Mahitaji | Maelezo ya Bajeti | Jumla ya Gharama (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Uhakika wa Mishahara ya Walimu | Mishahara ya walimu na wafanyakazi wote kwa mwezi ni takribani TZS 10,400,000. Kwa mwaka mzima, gharama hii ni TZS 124,800,000. | 124,800,000 |
| 2 | Upatikanaji wa Maji Salama ya Bomba | Gharama za utengenezaji wa miundombinu ya maji TZS 18,000,000 | 18,000,000 |
| 3 | Vifaa vya Kufundishia (Kompyuta na Internet) | Kununua kompyuta 20 kwa gharama ya TZS 1,500,000 kila moja na gharama ya huduma za intaneti kwa mwaka ni TZS 5,000,000. | 35,000,000 |
| 4 | Ufadhili kwa Uendeshaji wa Shule | Gharama za kuendesha shule kwa mwaka, ikiwa ni pamoja na mafunzo kwa viongozi na gharama zingine za usimamizi ni TZS 84,000,000. | 84,000,000 |
| 5 | Ujenzi wa Darasa la Ufundi Stadi | Gharama ya ujenzi wa darasa la ufundi stadi ni TZS 80,000,000. Pia, ununuzi wa vifaa vya kufundishia ni TZS 20,000,000. | 100,000,000 |
| | | **Jumla** | **361,800,000** |

Makisio ya bajeti iliyoanishwa ya mradi huu wa shule ni ya Mwaka mmoja ambapo itatumika kwa ajili ya kazi zilizoainishwa hapo juu. Aidha, mategemeo yetu michango hii inaweza kupatikana kupitia jamii, wafanyabiashara wakubwa wa ndani ya nchi yetu ya Tanzania, Makampuni kupitia CSR na watu wote ambao wataguswa na kituo hiki.

# Mazingira ya Shule


















# Hitimisho na Mapendekezo

Katika kumalizia, Kituo cha Bethsaida Orphanage Education Centre kinabeba jukumu muhimu katika kuboresha maisha ya watoto yatima na wale wanaotoka katika mazingira magumu nchini Tanzania. Kwa kutoa elimu bora, malezi, na msaada wa kijamii, kituo hiki kinachangia katika kujenga msingi imara wa maendeleo ya watoto hawa.

Hata hivyo, changamoto nyingi bado zipo, ikiwemo ukosefu wa rasilimali, vifaa vya kufundishia, uhakika wa mishahara ya walimu na wafanyakazi wa shule, na miundombinu bora. Ili kufanikisha malengo ya muda mrefu ya kituo, ni muhimu wadau mbalimbali washirikiane nasi, kuimarisha mifumo ya elimu, na kuendeleza ushirikiano wa kifedha.

Kwa kuwekeza katika watoto hawa, tunajenga jamii yenye nguvu na yenye uwezo wa kujitegemea. Hivyo basi, ni wajibu wetu sote kuhakikisha kwamba watoto yatima wanapata fursa sawa za elimu na maendeleo, ili waweze kujenga maisha bora na kuchangia katika ustawi wa taifa. Kwa pamoja, tunaweza kubadilisha maisha ya watoto hawa na kuwapa matumaini mapya kwa ajili ya kesho iliyo bora.

# Shukrani

Ni wajibu wetu kwa kila mtanzania kuwa sehemu ya kuwapenda na kuwajali watoto wetu ili Tanzania yetu ya kesho iwe bora ziadi ya leo. Mungu Ibariki Tanzania na wananchi wake.

Tuna kila sababu ya kumshukuru sana Mhe. Rais wetu Mpendwa wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Mama yetu Dkt. Samia suluh Hassan. Amekuwa wakati wote akituonyesha kwa vitendo dhana nzima ya uwajibikaji na kuwa sehemu ya kugusa maisha ya watu wengine. Sisi pamoja na kipato chetu kuwa kidogo sana lakini tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwa kuwezesha kubadilisha maisha ya watoto zaidi ya 417. Aidha, dhamira hii bado ni endelevu na tunakaribisha watanzania wengi zaidi waungane nasi katika safari hii yenye Tija kwa Taifa letu.

## Ni wajibu wetu kuhakikisha tunakuwa sehemu ya kuleta tabasamu kwa watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu.

---


## Contact

Bethsaida Secondary School
P.O.Box 5237, Dar es salaam
Tanzania
Mobile: +255 767228809

www.bethsaida.or.tz
www.bethsaida.ac.tz
info@bethsaida.ac.tz
facebook.com/bethsaidagirls